

Je WAJUA?

Watu bilioni 2 duniani kote hushuhudia hedhi. Wengi hushuhudia hedhi wakiwa kazini.

Hedhi au damu ya hedhi sio chafu, ukosefu wa usafi wala ya aibu.

Si sawa kwa mfanyakazi yeoye kudhulumu, kudhalilisha, au kufanya wengine kujisikia na wasiwasi kwa sababu ya hedhi.

Hakuna mfanyakazi anayepaswa kuwa kimya juu ya hedhi kwa sababu ya aibu au hofu.

Kila mtu anaweza kuchukua jukumu la kufanya hedhi jambo la kawaida.

V. KUIMARISHA HADHI NA HESHIMA WAKATI WA HEDHI

Mabingwa wa MHM wataimarisha aje hadhi na heshima kazini wakati wa hedhi?

Toa habari sahihi juu ya hedhi ili kupunguza imani hatari na zisizo sahihi.

Wahimize watu wazungumze juu ya hedhi (kama wanavyojsikia) na katisha tamaa ya uonevu na dhulumu zinazohusiana na hedhi.

Washauri wafanyakazi wapya juu ya jinsi ya kudumisha afya na usafi wa kutosha wa hedhi.

Zingatia jinsi MHM ambayo haitoshi inaathiri wafanyakazi na upendekeze hatua zifaazo kwa usimamizi.



Sikiliza wafanyakazi na utambue njia za kushughulikia na kukidhi mahitaji yao ya hedhi kazini; shirikiana na usimamizi.

Kusaidia wafanyakazi kupata bidhaa za hedhi, elimu ya hedhi, udhibiti wa maumivu, na miundo mbini inayodumisha MHM na heshima mahali pa kazi.


Waelekeze wafanyakazi kwa wataalamu wa afya na rasilimali zingine za kudumisha usafi wa hedhi (MHM) inapohitajika.



MWONGOZO WA KUDUMISHA USAFI WA HEDHI (MHM) YA MABINGWA WA MHM MAHALI PA KAZI



I. MZUNGUKO WA HEDHI



Urefu wastani wa muda wa mzunguko wa hedhi ni siku 28, lakini wawea kuwa tofauti kutoka kwa mtu mmoja hadi mwininge. Kwa kawaida, mzunguko wa hedhi wawea kuwa siku 21 hadi 35. Hedhi yawea dumu kwa kati ya siku 2 na 7 yaani siku ambazo utaona damu.

II. HEDI KAZINI

Hedhi inaweza kushughulikiwa kwa usalama na usafi kuititia bidhaa zifuatizo:

Ufahamu, kujithamini na taarifa kuhusu afya yao na usafi wa hedhi.	Ufikaji wa bidhaa salama na safi za ufyonyaji wa damu, iwe kazini au kwa bei nafuu karibu na mahali pa kazi.	KISODO CHA KUTUPWA KISODO KINACHOTUMIWA ZAIDI YA MARA MOJA KIKOMBE CHA HEDHI
Ufikaji wa sehemu salama na safi, zilizo na maji safi, sabuni na eneo murwa la kutupa bidhaa za hedhi.	Mazingira tegemezi ya kazi, yanayowawezesha kudhibiti hedhi bila uoga.	Wahimize wafanyakazi wanaoshuhudia hedhi ku:

III. MBIDHAZA ZA HEDHI

Bidhaa salama na safi ya hedhi, kama ifuatayo, inaweza kusaidia wafanyakazi kudhibiti hedhi yao mahali pa kazi:



Wahimize wafanyakazi wanaoshuhudia hedhi ku:

- Fuatilia tarehe ya kuanza na muda wa mzunguko wao wa hedhi.
- Chagua bidhaa za hedhi kuambatana na mtirirko wa hedhi.
- Beba bidhaa za ziada za hedhi, dawa za kukabiliana na maumivu, suruali, nguo na karatasii ya shashi (toilet paper).
- Epuka kutumia bidhaa zisizo na usafi kama vipande vya vitambara.
- Osha na kausha kabisa kisodo kinachotumiwa zaidi ya mara moja.
- Nawa mikono kwa kutumia maji na sabuni kabla na baada ya kushika bidhaa za hedhi.

Afya na usafi wa hedhi yaweza athiri afya na ustawi ya wafanyakazi walio katika hedhi, na uwemo wao wa kushiriki mahali pa kazi.



Tuunde mazingira tegemezi kwa wafanyakazi walio katika hedhi, na hivyo kuchangia mafanikio kazini.